

A KUIISHI KWA ROHO. Wagalatia 5:16, 18.

- ❖ Ina maana gani “kuenenda” kwa namna ya Mungu iliyo katika Biblia (Kumbukumbu la Torati 13: 4-5; Warumi 13: 13; Wakolosai 1: 10)?
- ❖ Mapenzi ya Mungu yameelezwa katika Biblia hivyo tunaweza “kuenenda” kwayo. Hii huhusisha kushika sheria zake na kanuni zingine zinazotusaidia kuisha vile Mungu anavyotutaka tuishi.
- ❖ Hata hivyo, kuzishika amri hizo ili tuokolewe sio namna yenyewe. Kile Mungu alichokifanya kinatosha kutuokoa.

B MAPAMBANO YA MKRISTO. Wagalatia 5:17.

- ❖ Tunapokea asili mpya tunapokubali kafara ya Yesu. Hiyo ni asili ya kiroho ambayo hupingana na asili ya “mwili” (Warumi 7:14-25).
- ❖ Lazima tuchague kumfuata Roho na kuung’ang’ania mkono wake wenye nguvu.

C MATENDO YA MWILI. Wagalatia 5:19-21.

- ❖ Paulo analinganisha kuishi kwa mwili na kuishi kwa Roho. Kuna tofauti za muhimu kati ya hivi viwili:
 - Cha kwanza kinahusu “matendo”, cha pili kinahusu “tunda”.
 - (1) Mwili *hudai* dhambi zetu na kutulazimisha kutenda dhambi.
 - (2) Roho *huzaa* tabia takatifu ndani yetu.
 - “Matendo” ni wingi “tunda” ni umoja.
 - (1) Asili ya dhambi huleta mgawanyiko, machafuko na kukosa umoja.
 - (2) Asili ya Roho huhamasisha umoja.
- ❖ Dhambi huvunja mahusiano ya watu na kuzalisha maumivu. Roho hurejesha mahusiano yetu na kuzaa uzima wa milele.

D TUNDA LA ROHO. Wagalatia 5:22-23.

- ❖ Upendo ni wa kwanza katika tunda la Roho, mengine hufuata.
- ❖ Upendo ni kipawa kinachotoa jumla ya amri kumi (Mathayo 22:35-40).
- ❖ Upendo hupingana na asili ya mwanadamu ya dhambi. Ndiyo maana upendo ni nembo kuu ya wale wanaomfuata Mungu.

E KUIISHI KWA ROHO. Wagalatia 5:24-26.

- ❖ Katika Wagalatia 5:16-26, Paulo alitumia vitenzi vitano kuelezea tunavyoongozwa na Roho.
 - Kuenenda [peripateō] (fg. 16): Lazima tutembe na Yesu kila siku tuishi naye.
 - Kuongozwa (fg. 18): Lazima turuhusu Roho atuongoze atuonyeshe wapi tuenda na tufanye nini.
 - Kusulubisha (fg. 24): Lazima tuifishe asili ya mwili na kuweka asili ya Roho.
 - Kuishi (fg. 25): Lazima tuzaliwe upya kila siku.
 - Kutembea [stoicheō] (fg. 25): Lazima tufuatishe nyayo za Roho na tuache aongoze maisha yetu.